# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

# SHULE YA SEKONDARI KASHISHI


**Namba za simu** SHULE YA SEKONDARI KASHISHI

**Mkuu wa Shule: 0768 488 039** S.L. P 170

**Makamu Mkuu wa Shule: 0788 688 090** ULYANKULU – KALIUA

**Matron: 0786 850 626** Tarehe: ……. /……./…………


Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi: ……………………………………………………………………..

S.L.P …………………………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KASHISHI,**

**HALMASHAURI YA KALIUA, MKOA WA TABORA MWAKA 2026**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2026, Tahasusi ya …………………. Shule ya Sekondari KASHISHI ipo umbali wa kilometa 155 kaskazini mwa mji wa KALIUA. Usafiriw a basi kutoka mjini KALIUA unapatikana katika kituo cha mabasi KALIUA nauli ni shilingi 15,000/= hata hivyo ili kurahisisha kufika kwa urahisi unashauliwa kupitia KAHAMA – SHINYANGA, ambapo utapanda mabasi ya Kwenda KALIUA katika kituo cha mabasi DODOMA na nauli ya shilingi 8,000/= hadi KASHISHI SEKONDARI.
   Muhul wa masomo unaanza tarehe …………………………. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………………….

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE YA SHULE**

a) Sare ya shule hii ni sketi mbili za linda box nyuma moja na mbele moja ubavuni linda tano ndogondogo kila upande ya rangi ya bluu nyeusi (Dark blue) kwa wasichana (ziwe ndefu zinazogusa vifundo vya mguu) na suruali mbili rangi ya bluu nyeusi (Dark blue) zisizobana (zisiwe modo) zenye linda mbili kiunoni kila upande kwa wavulana, mashati mawili meupe ya mikono mirefu kwa wavulana na wasichana (aje nayo).
b) Hijabu/Juba; rangi ya hijabu (Juba) ifanane na sare ya shule (Dark blue au nyeupe) aje nazo mbili.

c) Michezo: Sare za michezo ni pair ya jezi ya Taifa Stars yenye mistari ya bluu na njano kwa wavulana na wasichana jezi ya Zanzibar Heroes nyeusi na aje nayo.
Raba pair moja ya MICHEZO na aje nayo zisizo na visigino ya rangi NYEUPE kwa wasichana na NYEUSI kwa wavulana.
d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.
e) Soksi jozi mbili nyeupe (STOCKING) kwa wasichana na nyeusi jozi mbili kwa wavulana. Mkanda wa kuvalia suruali ni MWEUSI wa Ngozi (aje na mikanda miwili)
f) Sketi fupi za michezo (mini sketi) zinazofika magotini isiwe na linda, mshono wa solo, kitambaa aina ya Cretor rangi ya Bluu nyeusi (Dark blue).
g) Sweta blue nyeusi (Dark Blue) yenye V – Shepu.
h) Nguo za kushindia (shamba dress) T – shirt yenye nembo ya shule rangi ya kijivu yenye kora nyeusi, sketi mbili za linda box nyuma moja na mbele moja ya rangi nyeusi kwa wasichana (ziwe ndefu zinazogusa vifundo vya mguu na aje nazo. Wavulana ni suruali nyeusi mbili zisizobana aje nazo (isiwe modo) zenye linda mbili kiunoni kila upande zenye pindo chini (Turn Up) zenye size 15 miguuni.
i) Tai ndefu ya bluu nyeusi (dark blue) aje nazo mbili.
j) Ndala za kuogea rangi ya ugoro/nyeusi kwa wavulana aina ya RELAXO na rangi nyeupe /nyeusi kwa wasichana aina ya RELAXO.
**NB: NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI SHULENI KABISA** lakini kwa ajili ya baridi aje na Track suti bluu nyeusi (dark blue) isiyo ban ana isiyo kuwa na kofia, hivyo ukiweza mnunulie pair za kutosha za hiyo track suti na sweta za shule.

## 2.2 MICHANGO YA SHULE

a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni:-

| Na | Aina ya michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya SHULE A/C 51301100029 – KASHISHI SEC SCHOOL REVENUE COLLECTION, benki ya NMB. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye PAY SLIP na aje nayo akabidhi kwa MHASIBU)

b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta Shuleni ni:-

i. Unatakiwa kuja na vitabu japo kimoja kwa kila somo kulingana na Tahasusi uliyochaguliwa (orodha ya vitabu imeambatanishwa).
ii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa BIOLOJIA.
iii. Scientific calculator
iv. Godoro la sponji kwa ajili ya kulalia, futi mbili na nusu.
v. Mashuka pair 01, blanketi 01, foronya 01, chandarua 01 rangi ya pink kwa wasichana na rangi ya bluu Bahari (light blue) kwa wavulana ila yasiwe na maandishi.
vi. Vyombo vya chakula (kontena lenye vyumba vitatu, kikombe na kijiko).
vii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
viii. Kwanja 1.
ix. Mfagio wa ndani mmoja (soft bloom)
x. Passport size 4 za mwanafunzi
xi. Sanduku la chuma kwa ajili ya kuwekea nguo na vifaa vingine.
xii. Sabuni kwa matumizi ya mwanafunzi mwenyewe.
xiii. Koti jeupe la maabara.
xiv. Rimu moja kwa muhula
xv. Taulo kwa ajili ya kuogea ya rangi ya pink/light blue kwa wasichana na rangi light blue/pink kwa wavulana.
xvi. Ufagio wa cherewa 1 wenye fimbo.
xvii. Disposable gloves boksi moja kwa wanafunzi wa KEMIA na BIOLOJIA.

## 3. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga Mwalimu au mtu yoyote yule.
vi. Kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara, bangi Pamoja na matumizi ya aina yoyote ya madawa ya kulevya.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa, mahusiano ya mapenzi na mwanafunzi mwenzako.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi na redio pindi uwapo mwanafunzi (hutakiwi kuja na simu kabisa, SMART WATCH, FLASH)
xvi. Kudharau bendera ya Taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu, n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form), FOMU A – ambayo ijazwe na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai, FOMU B na FOMU C.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule, FOMU D.
d) Picha nne (04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanfunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja nan amba zao za simu.

5. Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
Karibu sana SHULE YA SEKONDARI KASHISHI.
**Saini ya Mkuu wa Shule……………………………………………………………….**
**Jina la Mkuu wa Shule: DOMINICK S. CHIKOMBO**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule…………………………………………….................................**

# KALIUA DISTRICT COUNCIL
# KASHISHI SECONDARY SCHOOL

## FOMU A: STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by a government medical Officer and returned to the HEADMASTER of KASHISHI SECONDARY SCHOOL.

To Medical Officer.
……………………………………………………
……………………………………………………
…………………………….………………
…………………………………………….

**Re: STUDENT NAMED ………………………………………………………….**
**FORM ……………. COMBINATION ………………….. AGE …………………..**
**SEX ……………….**

Please, examine the student mentioned above and comment on his/her health by responding to the following items:

1. Sight ………………………………………………………….
2. Hearing ……………………………………………………..
3. Speech ………………………………………………………
4. TB ……………………………………………………………...
5. Blood Pressure …………………………………………………
6. Pregnant for girls ……………………………………………..
7. Any other health problem …………………………………
8. Any physical disability ……………………………………….

Name and signature of medical officer
……………………………………………………
Designation ……………………………………………
Date ………………………………… Offical Stamp
…………………………………….

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

## SHULE YA SEKONDARI KASHISHI

**FOMU B**: HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi ………………………………………………………….
   Tarehe kamili ya kuzaliwa ………………………
2. Jina la baba ……………………………………………, Jina la mama
   ………………………………………………
3. Jina la mlezi ………………………………………..,
   anuani kamili ya mzazi/mlezi …………………………
4. Uhusiano wa mlezi ……………………………….,
5. kazi ya mzazi/mlezi (mkulima, mfanyakazi, mfanyabiashara)
   ………………………………………………
6. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni
   ………………………………………………..
7. Kama ni mkulima zao muhimu analotegemea ni ………………………………………..
8. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ni
   ……………………………………………………..
9. Afya yake (maelekezo kama mwanafunzi anayo matatizo ya kiafya)
   ………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………
10. Dhehebu ya dini ya mwanafunzi
    ……………………………………………………………………….
11. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi ni:

| | JINA KAMILI | UHUSIANO | ANUANI YAKE |
|---|---|---|---|
| 1. | ………………………………………. | ………………………………… | ……………………………… |
| 2. | ………………………………………. | ………………………………… | ………………………………. |
| 3. | ………………………………………. | ………………………………… | ………………………………. |
| 4. | ………………………………………. | ………………………………… | ………………………………… |

12. Uthibitisho wa mzazi/mlezi:
    Mimi ……………………………………………… nathibitisha kuwa maelekezo yaliyotajwa hapo juu ni sahihi.
    Anuani ya mzazi/mlezi ………………………………………….., Tarehe
    ………………………………

**FOMU C: KUKUBALI NAFASI (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)**

1. Jina la Mwanafunzi ………………………………………………………. (kama linavyo onekana kwenye RESULT SLIP).
2. Mimi ……………………………………………….. nimechaguliwa kuwa mwanfunzi wa shule ya Sekondari Kashishi. Nakubali nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Naamini kabisa kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo ili nijiendeleze kwa manufaa ya Watanzania.

   Hivyo ninaahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa shuleni, nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi. Ili kutimiza shabaha hii ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, MAARIFA, NIDHAMU YA HALI YA JUU NA UTII. Kwa viongozi wote kwa sheria na maelekezo yote yatolewayo na shule.

   Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapo husika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

   Sahihi ya Mwanafunzi: ………………………………………………… Tarehe: …………………………..

   **FOMU D: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI)**

   Mimi ……………………………………………………….. nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………………………., naahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi kwa mtoto huyu na kushirikiana na shule ikiwa Pamoja na kukubaliana na Sheria, Kanuni, Kulipa Ada, Michango na Maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule.

   Sahihi ya mzazi/mlezi ………………………………………………………..

   Tarehe ……………………

   **ILANI:**

   Mwanafunzi hatasajiliwa kama fomu A, B, C na D hazitajazwa kikamilifu.

ORODHA YA VITABU VINAVYOHITAJIKA

| SOMO | JINA LA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| FIZIKIA | i. PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL STUDENTS' BOOK FORM FIVE (2024), TIE – DAR-ES-SALAAM<br>ii. PRINCIPLE OF PHYSICS FOR CLASS XI<br>iii. Advanced Physics | i. TIE<br>ii. S. Chand<br>iii. Nelkon and Parker, 7th edition |
| BIOLOJIA | i. BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL. STUDENT'S BOOK FORM FIVE (2024)<br>ii. ADVANCED LEVEL BIOLOGY FOR FORM FIVE (5TH EDITION) | i. TIE<br>ii. CLEOPHACY J MAIGA |
| KEMIA | i. GENERAL AND INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS.<br>ii. PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL<br>iii. ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS. | i. TIE, 2024<br>ii. TIE, 2024<br>iii. TIE 2024 |
| ADVANCED MATHEMATICS | i. MATHEMATICS FOR | i. TIE |

| | | |
|---|---|---|
| | SECONDARY SCHOOL FORM FIVE<br>ii. ADVANCED MATHEMATICS | ii. C.J TRANTER |
| BASIC APPLIED MATHEMATICS | BASIC APPLIED MATHEMATIC FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL | TIE |
| GEOGRAPHY | i. PHYSICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS<br>ii. PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS | i. TIE, 2024<br>ii. TIE, 2024 |
| HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI | HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI, SHULE ZA SEKONDARI KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO | TAASISI YA ELIMU TANZANIA, 2024 |
| COMMUNICATION SKILLS | | TIE, 2024 |



**SARE YA DARASANI**



**SHAMBA DRESS**